


Mtumishi wa Mungu: Eng John James Ndindwa
**Subject:** MUHTASARI WA BIBLIA TAKATIFU
Contact: Email; ndindwajohn@gmail.com | Cell: 0717 401 569 |
Episode 1: The Bible Introduction

*"Yohana 1:1-3 Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.*

# UTANGULIZI KWA WASOMAJI WA BIBLIA

Bible kwa kiingereza na kwa Kigiriki Biblia (*Kilipojia Kiswahili*), linalomaanisha "vitabu," jina ambalo katika karne ya tano lilianza kutolewa kwa mkusanyiko mzima wa vitabu vitakatifu, "Maktaba ya Ufunuo wa Kimungu." Jina Biblia lilikubaliwa na Wickliffe, na polepole likaja kutumika katika lugha yetu ya Kiingereza.





Biblia ina vitabu sitini na sita tofauti, vilivyotungwa na waandishi wengi tofauti, katika lugha tatu tofauti, chini ya hali tofauti; waandikaji wa karibu kila vyeo vya kijamii, wakuu wa serikali na wakulima, wafalme, wachungaji wa mifugo, wavuvi, makuhani, wakusanya-kodi, watengeneza mahema; wenye elimu na wasio na elimu, Wayahudi na Wamataifa; wengi wao hawajulikani wao kwa wao walioandika katika vipindi mbalimbali katika muda wa miaka 1600 hivi: na bado, baada ya yote, ni kitabu kimoja tu kinachoshughulikia somo moja tu katika nyanja na mahusiano yake yasiyo na idadi, somo la ukombozi wa mwanadamu.

Biblia ina mweleza Mungu pande zote kwa wanadamu. Biblia ni ufunuo wa Mungu ulioandikwa kuhusu mapenzi ya Mungu kwa wanadamu. Biblia ni kitabu zaidi ya, kuliko kitabu kingine chochote. Biblia ni kitabu cha ajabu!


Ni kitabu cha Vitabu,kitabu kilichovuviwa,ni kitakatifu kwa sababu kina maneno ya mwandishi mkuu ambae ni mtakatifu.Ni kitakatifu kwa sababu mjumbe wake ni mtakatifu,maandiko yake ni matakatifu! Ni kitakatifu kwa sababu maudhui yake ni kutufanya kuwa watakatifu.

Biblia ina vitabu 66 vilivyoandikwa na waandishi 40, kwa muda usiopungua miaka 1500; (yaani kuanzia 1400 K.K hadi 100 B.K). zaidi ya vizazi 40, katika mazingira tofauti,wakati tofauti,nyakati tofauti,ktk mabara 3(asia,ulaya na Afrika) ktk lugha 3 (kiebrania,kiaramu na kiyunani) Karibu Agano la Kale lote liliandikwa kwa lugha ya Kiebrania isipokuwa mafungu machache kwenye kitabu cha Danieli yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiaramu. Agano Jipya limeandikwa kwa lugha ya Kigiriki/kiyunani.


Sasa, mwanzoni mwa mwaka 2007; Biblia nzima tayari imekwishatafsiriwa kwa lugha tofauti yaani. 429 Na Agano Jipya au Agano la Kale tu zimekwishatafsiriwa kwa lugha tofauti 1144. Na Biblia nzima tayari imekwishatafsiriwa kwa lugha za Afrika mia moja sitini. (160) Steven Lagton (1228) Aliigawanya Biblia ktk sura. R Nathan (1488) aliigawanya agano la kale katika aya na Robert Stephanus(1551) aliigawaya Agano jipya katika aya. Biblia ilikuwa kitabu cha kwanza kuchapishwa na machine mwaka 1455 na Johann Gutenberg

Vitabu vingine huchakaa lakini kitabu hiki Biblia hupita juu ya karne zote. Vitabu vingine lazima vibadilishwe kufuatana na umri. Bali wazee kwa vijana huipenda Biblia. Vitabu vingi ni kwa ajili ya sehemu ndogo ya watu na huwavutia watu wa lugha ile tu, lakini kitabu hiki Biblia, sivyo.

- Katika Biblia kuna vitabu 66. Katika Agano la Kale kuna vitabu 39 na katika Agano Jipya 27.
- Katika Biblia kuna sura 1,189; Agano la Kale kuna sura 929.Na Agano Jipya 260.
- Katika Biblia ya kiswahili kuna mistari 31,102. Ambazo ni mistari 23,145 katika Agano la Kale. Na mistari 7,957 katika Agano Jipya.
- Wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu. (2 Petro 1:21).






AGANO LA KALE

- Kuna vitabu 5 vya Sheria( Pentatuki);

Mwanzo, Kutoka, Mambo ya walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati.

- Vitabu 12 vya historia.

Yoshua,Waamuzi,Ruthu,I Samweli, II Samweli,I Wafalme,II Wafalme,I Mambo ya Nyakati,II Mambo ya Nyakati, Ezra,Nehemia na Esta.

- **Vitabu 5 vya mashairi;**

Ayubu,Zaburi,Mithali,Mhubiri na wimbo ulio bora!.
Vitabu 17 vya unabii

- **Manabii wakubwa 5:**

Isaya,Yeremia,Maombolezo,Ezekieli na Danieli.

- **Manabii wadogo 12;**

Hosea,Yoeli,Amosi,Obadia,Yona,Mika,Nahumu,Habakuki,Sefania,Hagai,Zekaria na Malaki


- **Kwa maelezo zaidi ni kuwa;Katika Agano la Kale.**

Kitabu cha katikati ya Biblia : Mithali; Sura ya katikati : Ayubu 29; Aya ya katikati : II Mambo ya Nyakati 20:17; Aya ndefu zaidi : Esta 8:9; Aya ya katikati katika Biblia nzima : Zaburi 118:8; Sura ndefu zaidi : Zaburi 119; Sura fupi na ya katikati mwa Biblia : Zaburi 117.
Tunaweza kuwaza kwamba Agano la Kale ni kama msingi. Na Agano Jipya ni kama jengo juu yake. Msingi haufai kama jengo halijengwi juu yake. Jengo haliwezekani kama msingi haupo. Kwa hiyo Agano la Kale na Agano Jipya hutegemeana.

Kama unasoma Agano la Kale tu au Agano Jipya tu, ni sawa na kuruka kwa mguu mmoja. Agano la Kale ni kama mguu mmoja na Agano Jipya mguu mwingine. Ikiwa unatembea kwa miguu miwili, basi unakwenda vizuri.

AGANO JIPYA




- Vitabu: 27; Sura: 260; Aya: 7,957; Waandishi : 8 ; Kitabu cha katikati : 2Thesalonike
- Sura ya katikati: Warumi 13: Aya ya katikati : Matendo 17:17: Aya fupi? Kitabu kirefu: Luka; Kitabu kifupi: 2 Yohana.
- Kitabu vya mwanzoni kabisa kuandikwa ni II Thesalonike,Yakobo,Wagalatia, cha mwisho NI ufunuo Wa Yohana.
- Vitabu vya Agano Jipya tunaweza kuvipanga hivi: Injili Vitabu 4 – MATHAYO, MARKO, LUKA na YOHANA.
- Historia – kitabu 1, MATENDO YA MITUME. Nyaraka 21.
- Paulo aliandika nyaraka 13 ama 14,

- Warumi,I Korintho,II Korintho,Wagalatia,Waefeso,Wafilipi,Wakolosai,I Thesalonike,II Thesalonike,I Timotheo,II Timotheo,Tito,Filemoni ( Waebrania);
- Nyaraka nyingine 7; Yakobo, I Petro,II Petro,I Yohana,II Yohana,III Yohana, Yuda.
- Hatujui, ni nani hasa aliandika waraka wa WAEBRANIA (pengine ni Paulo),
- Kitabu cha unabii – kimoja – UFUNUO.

ANGALIZO:
Biblia ya kiyahudi ina vitabu 51 tu! Agano la kale 24 na Jipya 27. Kwanini.? @ vitabu vya manabii wadogo12 vimekusanywa na kuwa kitabu kimoja,vivyo hivyo kwa Ezra-Nehemia,Mambo ya Nyakati,wafalme na Samweli zote mbili,

Biblia ya Roman Catholic (Vulgate) INA vitabu 72 kutokea vitabu 80 vya awali,vitabu 46 Agano la kale na 27 agano jipya..hii NI kutokana na kuvikubali vitabu vya apokrifa; Tobithi, Judithi, Hekima ya Yoshua bin Sira, Baruku, Makabayo wa 1&2, na hekima za Sulemani pia Danieli sura 13 &14,Esta sura za mwishoni.

Hivyo maandiko katika Biblia zanaweza kuwa sawa kasoro itaonekana kwenye vitabu nyongeza na sura nyongeza!

## USOMAJI WA BIBLIA NA UCHAMBUZI WA MAANDIKO

NI mengi yaliyoandikwa duniani,mamilioni ya vitabu,magazeti,majarida, na masomo mbalimbali yahusuyo mambo mbalimbali katika dunia yetu. Biblia NI Neno la Mungu lililovuviwa na kuleta tofauti kubwa kati ya kitabu Biblia na vitabu vingine vyote. Ndani ya kitabu hiki Biblia kuna maneno makuu mawili yanayo eleza moja ya sifa kuu ya Biblia yaani Neno la Mungu.
*1. Neno la kiyunani "logos"*
*2. Neno la kiyunani "Rhema"*

Maneno haya hutumika sana katika usomaji na kuelewa uzito Wa andiko,uvuvio wake na ukuu wake.
Neno "logos" humaanisha yaliyoandikwa! yaani kumbukumbu fulani juu ya kila unachotaka kujua,habari zake zilisha andikwa. mfano; Yesu akamjibu shetani " imeandikwa, MTU hataishi kwa mkate tu! (logos).
Neno la pili " rhema" humaanisha lililokusudiwa,vuviwa kwa majira na kwa wakati huu! mfano; "Bali kila neno litokalo kinywani mwa BWANA!( rhema) ndio maana tangu enzi na Torati hadi na leo,Biblia imekuwa ikisomwa na Neno likihubiriwa ama kufundishwa lakini ujumbe wake haujaisha,hauja chakaa,hajapitwa na wakati,unawafaa watu wote,maususi kwa kila jambo,tukio na kuwa na nguvu ya kuathiri jamii,MTU na taifa unaposikilizwa!

Wahubiri wakubwa waliowahi kuhubiri sana, mfano; Billy Graham,Catherine Kuhlman, Bonke,Myles,Benny,Maxwell nk, hata ikatokea wakakutembelea Leo nyumbani kwako, utashangaa atasoma Mathayo ama Hosea sura na aya /mistari ile ile usomayo kila siku! Nitakushangaa sana ikiwa kwa kujiona unajua,unaelewa sana maandiko,umekomaa kiroho,wewe NI mshirika Wa Siku nyingi kanisani; hutaki kuonywa, kusahihishwa, kupewa ushauri eti kwa sababu hilo andiko wanalokusomea unalijua,'nilijua tu utanisomea hilo andiko' (logos). Hii ni sawa na kusema umefikia level ya kuipita Biblia hivyo hakuna jipya usilolijua!  " Neno la Mungu li hai...." (rhema)

Uchambuzi Wa Biblia/maandiko!

Shule za sekondari wanafundisha juu ya tahakiki,yaani uchambuzi Wa vitabu vya Riwaya,Tamthilia na ushairi. Kwa namna kwamba mwanafunzi hupaswa kukisoma kitabu fulani,kisha akakielezea kwa kuchambua NANI mhusika mkuu,hadhira yake,maudhui yake,dhima kuu ya kuu,mada mbalimbali Ndani yake nk. Hivyo NI sawa na kueleza alivyokielewa kwa muhtasari kitabu hicho!Kadhalika kwa Biblia njia kama hii unaweza kuitumia kuielewa na kuvielezea vitabu vya Biblia!

Kuoanisha na kuonesha nini wazo kuu katika kitabu cha mwandishi,sura hii na nyingine katika Biblia. Kutafsiri/kufasiri maandiko hakuji kwa namna tunavyo taka sisi bali atakavyo Mungu! Epuka kujilisha/kuwalisha watu tango pori!

Kuna kanuni zenye kubeba funzo kuu (Doctrine) za maandiko na kuna kanuni za mahubiri ya kawaida Mfano: mafunzo juu ya utakatifu huhusisha toba ya kweli,kuonya juu ya dhambi! nk. Kwa upande wa mahubiri juu ya mafanikio! Huusisha mambo kama utoaji, panda na uvune Baraka yako. Hivyo lazima mkazo uwe kwenye kanuni kuu za mafundisho ili MTU/watu waelimike sio kumsisimua. Biblia Neno la Mungu lina kina,urefu,upana na kimo ambacho mpaka sasa bado hatujakifikia pengine hata robo yake!

Soma sana, soma tena,tafakari,chambua,fafanua na ishi(direct application) ya ulichojifunza"Nataka nimjue Yesu,na nizidi kumfahamu, Mapenzi yake nifanye Yale yanayompendeza!"

## HISTORIA YA BIBLIA KATIKA KUTAFSIRIWA KATIKA LUGHA MBALIMBALI!

"Gombo la chuo" NI neno lililotumika sana katika Agano la kale,likimaanisha maadiko matakatifu.Sehemu ama jumla ya maandiko ya nabii Fulani ama torati! Huitwa chuo,."Chuo" ni neno lingine lililokuwa likimaanisha maandiko yaliyokuwa yanaandikwa katika ngozi laini,na kusokotwa kwa kuviringisha wakati unasoma ama unafunga ili kuhifadhi maandiko hayo!.

*Yeremia 36:2 Twaa gombo la chuo, ukaandike ndani yake maneno yote niliyokuambia juu ya Israeli, na juu ya Yuda, na juu ya mataifa yote, tangu siku ile niliponena nawe, tangu siku za Yosia, hata siku hii ya leo.*

Mfano; chuo cha nabii Isaya. Biblia NI mkusanyiko Wa chuo mbalimbali,yaani torati,manabii,Injili, na nyaraka. Hivyo wakati mwingine wako waliozoea kusema Gombo la chuo akimaanisha kitu kilekile! Lakini vitabu vyote 39 vya Agano la kale viliandikwa kwa kiebrania! Na vile 27 vya Agano Jipya viliandikwa kwa kiyunani! Je ikawaje sasa Biblia ikatafsiriwa kwa lugha mbalimbali hadi za makabila ya watu?

*Matendo ya Mitume 8:28 akawa akirejea, ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya.*

Ooh! Haikuwa kazi ndogo hata kidogo,wako waliochomwa kama nyama za mshikaki wakafa. kisa na mkasa wametafsiri Biblia kwa lugha isiyoruhusiwa!

**SASA TUONE ILIVYOKUWA HAPO ZAMANI ZA KALE**

Mnamo mwaka 250 K.K pale Alexandria Misri,jopo la watu 72 lilikusanyika kutafsiri Biblia kutoka kiebrania kwenda kiyunani! Waliongeza vitabu 14 vya Apokrifa kwenye vitabu vile 39 vya Agano la kale. Mwaka 382 B.K Jerome alitafsiri Biblia kwenda Kilatini akiviweka na vitabu vile visivyo rasmi,vitabu 14 vya Apokrifa hivyo Biblia aliyoitafsiri(Vulgate) ikawa na vitabu 80.






Chini ya utawala Wa Mapapa Wa kanisa la Roman Catholic walipiga marufuku kufasiri/kutafsiri Biblia kwenda lugha zingine isipokuwa kilatini tu. Mwaka 1384 John Wycliffe Profesa wa Oxford,mwana zuoni na mtheologia! akamwa MTU Wa kwanza kuitafsiri Biblia kwenda lugha ya kiingereza! Alinakili mkono kwa mkono,yaani teknologia ya kuchapisha ilikuwa bado haijavumbuliwa. Miaka 44 baada ya kifo chake,nakala kadhaa za maandiko yake yakamfikia Papa,alikasirika sana, kusikia kuna MTU mmoja aliyetafsiri Biblia kwenda kiingereza! Aliamuru kaburi lake lifukuliwe,mifupa yake ipondwepondwe kisha itupwe mtoni. Mtu yeyote aliyekutwa,ama kukamatwa na nakala zozote za Biblia zisizokuwa kwa kilatini,walihukumiwa hukumu ya kifo. mwaka 1415 B.K, kama vile utani, mwanafunzi Wa John Wycliffe, John Hus alikamatwa akiwa na nakala kadhaa ambazo zilitumika kumchoma kama mwizi mbele ya kadamnasi ya watu. kabla hajafa akasema maneno haya ! Namnukuu.

""Kwa miaka 100 ijayo Mungu atamwinua MTU, ambae wito wake kwa mageuzi hauwezi kuzuiliwa!""" .mwisho Wa kumnukuu!

Kama alivyotabiri mwaka 1517 B.K, Martin Luther akaanzisha mageuzi ya wazi dhidi ya kanisa Katoliki kwa kugongelea mlangoni mwa kanisa,wakati kabla ya misa/ibada kuanza,mambo 95 kinyume na Neno la Mungu yanayofanywa na Kanisa katoliki mjini Wittenberg! kitabu cha Foxe kilichokuwa kikiandika mashahidi Wa Imani(wafia dini) waliouwawa kwa kosa la kulipinga,ama kwenda kinyume na kanisa Katoliki;kilieleza mwaka huo Wa 1517 watu 7 walichomwa hadharani kwa kosa la kuwafundisha watoto wao kusali sala ya Bwana kwa lugha ya kiingereza/kimombo badala ya kilatini.

Martin Luther aliendа mbali zaidi katika kuitafsiri Biblia kwenda kijerumani huku akihimiza kila MTU asome Biblia mwenyewe! Asisubiri kusomewa kanisani. Mwaka 1450 huko Mainz,Ujerumani Johann Gutenberg akawa MTU Wa kwanza kutengeneza mashine ya kuchapisha Biblia! Ikarahisisha Biblia kunakiliwa kwa haraka,na kusambazwa kwa kasi,tofauti na hapo kabla! ambapo nakala za Biblia zilikuwa chache na ziliuzwa ghali sana! Matajiri tu ndio walioweza kununua. William Tyndale, mwana zuoni,mbobevu tena kapteni Wa jeshi la mageuzi alikuwa anazungumza lugha 8 tofauti kwa ufasaha kana kwamba ndizo alizozaliwa nazo! Alichapisha Biblia(Agano Jipya) kwa lugha ya kiingereza. Alitumia karibu miaka 11 kuikamilisha Agano Jipya kwa lugha ya kiingereza, akinakili kutoka kwa Erasmus aliyewahi pia kutafsiri Agano Jipya kutoka Kiyunani kuja kilatini!

Mwaka 1530 kazi yake ilipata soko sana kwa sababu kila MTU alitaka apate nakala yake! Hivyo zilifichwa kwenye mabarota ya pamba na magunia ya unga kama bidhaa za magendo ili ziwafikie Wateja wake! Ambao wengi walikuwa watumishi Wa Mfalme. Kila aliyekamatwa na kopi/nakala hizo alihukumiwa kufa,la sivyo aiteketeze kwa moto kabla hajakamatwa! Maparoko,mapadri walizitafuta nakala hizo kwa waumini wao ili kuwazuia wasizisome kwa madai zilikuwa na makosa mengi! na ndugu Tyndale alitafutwa kwa udi na uvumba, Mwisho nakala hizo zilifika hadi chumbani mwa Mfalme Henry VIII Wa Ungereza. Mwaka 1536 William alikamatwa baada ya kusalitiwa na rafiki yake,akafungwa kwa siku 500,kisha akanyongwa na akachoma moto hadi kuwa majivu.

Kabla hajafa akasema " Ee Bwana naomba ufungue macho ya Mfalme Wa Ungereza"!. Mwisho Wa kumnukuu. Miaka 3 baadae Mfalme Henry VIII akatoa amri,akaidhinisha mchakato Wa kuitafsiri Biblia yote kwa kiingereza iliyopewa jina la 'Biblia kubwa' chini ya Askofu Thomas Cranmer Wa jimbo la canterbury alimteua Myles Coverdale kuichapisha biblia hii iliyokuwa na kimo cha inchi 14! Kuanzia April 1539 hadi Desember 1541 yalichapishwa matoleo 7 ya Biblia hii. John Calvin mwana zuoni,mthelogia,mwenye fikra za mageuzi, huko Geneva uswizi alianzisha chuo cha Biblia na John Knox Wa Scotland walisimamia mpango Wa Biblia iliyoitwa "Geneva study Bible" ilikusudiwa kuwafundisha watoto wao wakati wao wako uhamishoni,ama kifungoni! Ilikuwa Biblia ya kwanza kutumia Sura/mlango na aya/mstari kila ukurasa ukiwa na mistari 42! kwa kipindi cha miaka 100 iliongoza kuwa bora zaidi ya nyingine! Ilikuwa ya kwanza kupelekwa bara la Amerika.

Mwaka 1560-1644 matoleo 144 yalichapishwa katika juhudi ya kuboresha na kuihakiki maana halisi ya kila neno likilotumika kuitafsiri. Mwaka 1611 NI mwaka Wa historia kubwa katika Biblia kwani mfalme James VI alifadhili mpango Wa kuchapisha Toleo la Bibli litakalomaliza ubishi na kuwa bora kuliko yote yaliyopita. Miaka 6 ilitumika kuikamilisha! Mwaka 1605 -1606 utafiti ulifanyika, 1607-1609 uchambuzi na kuikusanya 1610 kuichapisha, 1611 ilikamilika yenye urefu Wa kimo inchi 16 kwa ukubwa. Ndio hadi Leo inatumika kama standard ya nyingine zinazotafsiriwa!

- Zingine zilizochapishwa 1885 ilichapwa tena
- 1971 new American standard Bible (NASB)
- 1973 new international version (NIV)
- 1982 new king James version (NKJV)
- 2002 English standard version (ESV)
- Biblia kwa lugha ya kiswahili, Union Version (SUV) ilichapwa kwa mara ya kwanza mwaka 1952, 1997: na lugha iliyotumika inajulikana kama kiswahili cha kimvita! na Kiunguja. Ndio maana maneno kama "maseyidi,"mashehe," yametumika! Na sinagogi wakitafsiri kama sinagogi la wayahudi!
- Japokuwa Mbingu na nchi zitapita! Neno la Mungu ladumu hata milele!

*Luka 21:33 Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.*

***SOMO HILI LITANDELEA, BWC WANAKUSUDIA KUWA NA SHULE YA WATUMISHI AMBAO WATAKUWA WANAFUNDISHA WATENDA KAZI WAWEZE KUFAHAMU HISTORIA YA IMANI YETU.***